

# ‘MAJIBU YENYE FAIDA’

NO.8

# KUHUSU

## MASWALI YANAYOFUNGAMANA NA MIFUMO MIPYA

# **MTUNZI, SHEIKH SWALEH BIN FAWZAN AL FAWZAN**

# MFA SIRI ABUL 'AALIYAH 'UMAR BIN MUHAMMAD KONDO

# PONGWE - TANGA - TANZANIA

**Swali la tisa:** Je..!kuna ubaya wowote katika kutahadharisha haya makundi yanayokwenda kinyume na manhaji (njia) ya Ahlus-sunna waljama'ah ?

**Jawabu:** Sisi tunawatahadharisha wenyе kukhalifu (kwenda kinyume) wote kwa ujumla, na tunasema. Tunalazimiana na njia ya Ahlu-s-sunna waljama'ah, na tunamwacha yeьте atakaewakhalifu Ahlu-s-sunna waljama'ah ni mamoja uwe mukhaalafa mkubwa au mdogo, kwa sababu sisi tutakapozembea katika jambo lolote linalokwenda kinyume (na manhaji) litaendelea kukua kidogokidogo na litakuwa kubwa, basi kukhalifu hakufai milele.

Na kunapasa (ni wajibu) kulazimiana na njia ya Ahlu-sunna waljama'ah katika kubwa na dogo.

**Swali la kumi:** Je..! inatulazimu sisi kuyataja mema ya yule tunaemtahadharisha katika wao?

**Jawabu:** Yatakapotajwa mema yao maana yake wewe umelingania kuwafuata wao,hapana,hatutayaja mema yao.Taja kosa ambalo wanalo tu,kwa sababu wewe hukuwakilishwa kuwasifia walivyo,wewe umewakilishwa kubainisha kosa ambalo lipo kwao ili watubie kutokana na kosa hilo ili wengine watahadhari nao,na kosa ambalo wako nalo, huwenda likaondoka na mema yao yote iwe kufru au shirki,na huwenda (kosa) likazidi mema yao ,na huwenda yakawa mema kwa mtazamo wako wewe na si mema mbele ya Allah.